

**Issue no:** 01 | **Vol no:** 06 | **september** 2025: 44-55

# Matumizi ya Blabu kama mtindo wa kuakisi maudhui: Mfano wa riwaya ya *Utengano* na *Chozi La Heri*

**Phillis Ang'ayi Ong'ale** [1]
**Beverlyne Asiko Ambuyo** [2]
**Benard Odoyo Okal** [3]

(**1.2.3**) **Maseno University, Kenya.**
Main author's email: phyllwayne@gmail.com

**Article History**
Received: **2025.07.11**
Accepted: **2025.08.13**
Published: **2025.09.12**

**Cite this article in APA**
Ong'ale, P. A., Ambuyo, B. A., & Okal, B. O. (2025). Matumizi ya *blabu* kama mtindo wa kuakisi maudhui: Mfano wa riwaya ya *Utengano* na *Chozi la heri*. *Editon consortium journal of kiswahili*, *6*(1), 44-55. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v6i1.621

**Ikisiri**
Upekee katika uundaji wa kazi ya fasihi huitwa mtindo na hutofautiana kutoka mwandishi mmoja hadi mwingine. Mtunzi huchagua mtindo wa kueleza kazi yake unaodhihirika ndani ya kazi hiyo na pia kupitia jalada la mbele na nyuma. Kimsingi, jalada la mbele huwa na ishara mbalimbali huku la nyuma likiwa na blabu. Wahakiki wengi huchambua majalada hayo kwa kutaja ishara na kuzihusisha na matukio kitabuni moja kwa moja bila kuzingatia nadharia yoyote. Wengine huchambua jalada la mbele na kupuuza lile la nyuma lililo na blabu lenye mtindo wake wa kimuundo na kiisimu. Kutokana na udhaifu huu, utafiti ulilenga kuonyesha matumizi ya blabu kama mtindo wa kuakisi maudhui katika riwaya teule za Kiswahili; *Utengano* (Mohammed, 2009) na *Chozi La Heri* (Matei,2014). Nadharia ya Muundo Kipera ya Swales (1990) na pia maoni ya Valor (2005) yalitumika. Utafiti ulizingatia muundo kiuchanganuzi na kufanyika maktabani. Usampulishaji wa makusudi ulitumika na sampuli ni riwaya ya *Utengano* (Mohammed, 2009) na *Chozi La Heri* (Matei, 2018). Data zilikusanywa kupitia mbinu ya unukuzi kwa kutumia orodha ya uchunzaji. Data ilichanganuliwa kimaudhui na kuwasilishwa kwa maelezo ya kinathari. Matokeo ya utafiti yalionyesha misogeo-hatua minne katika blabu za riwaya teule; utangulizi, kuhusu mwandishi, kampuni ya uchapishaji na maudhui kutoka kitabuni. Maudhui kutokana na misogeo-hatua ni utengano, mabadiliko, tamaa na ukabila. Elementi za kiisimu za mshikamano zilizobainishwa ni ubadilishaji, uunganishaji, urejeshi, udondoshaji na hiponimu. Utafiti utasaidia katika uchambuzi wa blabu za kazi za fasihi ya Kiswahili kinadharia. Watafiti wa baadaye wanaweza kutafiti vipengele vingine vya kiisimu katika blabu za tamthilia.

**Maneno muhimu**: Blabu, jalada, mshikamano, msogeo-hatua, muundo kipera.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

**UTANGULIZI**

Wamitila (2003) anasema kuwa blabu ni muhtasari mdogo wa maudhui ya kazi ya kifasihi ambao huandikwa na mchapishaji katika jalada la nyuma la kitabu. Anasema kuwa blabu hujaribu kutaja sifa muhimu na za kipekee za kazi inayohusika kama njia ya kuwashawishia wasomaji na wanunuzi. Chanzo cha dhana na matumizi ya blabu imehusishwa na waandishi na nyakati mbalimbali. Kulingana na Wikipedia, neno hili lilianzia Ujerumani na mchapishaji Robert mwaka wa 1902. Hata hivyo katika uandishi wa bibliografia za kijerumani, blabu hupatikana katika ukurasa wa pili wa kitabu husika chini ya anwani kuu au kwenye jalada la nyuma.

Wengine wanadai kuwa neno hili lilitokana na mwandishi Matthews Brander mwanzoni mwa mwaka wa 1922. Mwandishi huyu, katika makala yake ya '*A round up of Blurbs New York Times (*1922*)* anadai kuwa dhana hii ilivumbuliwa na Gellet Burghes. Anasema kuwa Gellet alitoa ufafanuzi wa neno hili kama maelezo ya mchapishaji kuhusu kitabu cha mwandishi fulani ambayo ni utambulisho wa kazi hiyo pamoja na wahusika (Matthew, 1922). Gellet Burghes alikuwa mcheshi mmoja wa Kimarekani na alizungumzia blabu mwaka wa 1907 ili kukuza kitabu chake kiitwacho *Are you a Bromide?*(*1906).* Aliunda jalada ambalo lilikuwa na picha ya mwanamke aliyeitwa 'Belinda Blurb' ambaye alikuwa amefungua kinywa kana kwamba anapiga kelele. Kitendo hiki alikiita '*blurbing*'. Hapo mwanzo, neno hili lilitumika kuonyesha lugha yenye sifa nyingi iliyotiwa chumvi na yenye kuibua fikra hasi. Burghes anasema kuwa alitumia neno hili kukejeli sifa zilizowekwa kwenye jalada la nyuma.

Japo dhana ya blabu imekuwepo kwa miongo kadhaa, utafiti wa kiakademia kuhusu dhana hii umepata mwamko mpya hivi majuzi hivyo kupelekea kuwepo kwa mitazamo mbalimbali kuihusu kama ilivyo katika kazi za wataalamu mbalimbali. Miongozo mingi ya wahakiki wa kazi za fasihi haijashughulikia jalada la nyuma lililo na blabu. Kunao waandishi mbalimbali ambao wameandika miongozo ya uchambuzi wa riwaya mbalimbali bila kutaja chochote kuhusu blabu za riwaya hizo. Mathalan, Kitula (2008) alishughulikia uchambuzi wa riwaya ya *Utengano* (Mohammed, 2009) kwa kurejelea anwani, muundo wa riwaya, dhamira na mengineyo pasi kutaja chochote kuhusu jalada la nyuma lililo na blabu. Japo huenda uchambuzi wa blabu haukuwa madhumuni yake, ni jambo la busara kuzungumzia blabu kwani huangazia kwa haraka ujumbe uliomo kitabuni. Naye Kitula (2001) alihakiki riwaya ya *Kiu* moja kwa moja kuhusu dhamira, maudhui, wahusika na mitindo ya uandishi. Hakuna kinachoangaziwa kuhusu blabu la riwaya hii. Mathenge (2006) katika *Mwongozo wa Kifo Kisimani* alichambua jalada la tamthilia hiyo kwa kurejelea michoro na rangi mbalimbali. Amehusisha rangi na picha hizo na matukio yanayopatikana katika tamthilia hiyo moja kwa moja bila kuhusisha nadharia yoyote wala kushughulikia jalada la nyuma lililo na blabu. Hivyo basi, uchanganuzi wa blabu haujatiliwa maanani sana katika uhakiki wa kazi mbalimbali (Pupipat, 2023).

Mbali na pengo la kinadharia, baadhi ya tafiti kuhusu blabu za kazi za kifasihi hazijahusisha masuala mengine pia kama vile mshikamano. Dai hili linaangaziwa na Banari et al. (2019) ambao wanasema kuwa japo tafiti zimefanywa kuhusu msogeo hatua katika uchanganuzi wa blabu, masuala mengine kama vile mshikamano wa kileksika na kisarufi aghalabu hayajashughulikiwa. Mshikamano au ushikamano ni uhusiano mzuri wa kisarufi na kileksika baina ya elementi za matini. Elementi hizi zinaweza kuwa maneno, kishazi, sentensi na hata pia aya. Masuala ya mshikamano yalidokezwa pia na Valor (2005) na Sari (2018) kuwa mbali na mtindo na ujumbe kwenye blabu, mambo ya kiisimu vilevile hufaa kuangaziwa. Atai na Aghari (2017) wanasema kuwa kama muhtasari wa maneno yanayosifia kazi bunifu, blabu huwa na mtindo wa kipekee unaoweza kujumuisha matumizi ya msamiati uliyopigwa chuku, na sentensi mbalimbali ambazo lazima ziwe na athari fulani kwa msomaji.

Aidha blabu huwa na mchango wa kisarufi ambao husaidia pakubwa katika uundaji wake. Ni kutokana na pengo hili ambapo utafiti ulichunguza blabu kama mtindo wa kuakisi maudhui katika kazi teule za fasihi kwa kuonyesha namna misogeo-hatua katika blabu ilivyojenga maudhui katika riwaya ya *Utengano (*Mohammed, 2009) na *Chozi la Heri (*Matei, 2014) kwa kurejelea nadharia ya Muundo kipera na kuonyesha namna masuala ya mshikamano ama wa kileksika au kisarufi hujitokeza katika ujenzi wa blabu.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Kathpalia (1997) alifanya utafiti wa kulinganisha blabu za vitabu vya wachapishaji wa kimataifa na wale wa Singapore ambapo alionyesha umuhimu wa utamaduni wa kijamii katika kugawanya aina za blabu. Vitabu kutoka makundi yote mawili yalionyesha sehemu nne za

uandishi wa blabu kama vile kuthibitisha kitabu, kuthamini kitabu, kuonyesha hati, uungwaji mkono na ulengaji hadhira.

Bhatia (2014) alieleza blabu za vitabu vya kiakademia kwa kurejelea hatua tano katika uandishi wa blabu ambazo ni anwani, somo au funzo, kuthamini kitabu, kulenga hadhira na kuonyesha hati. Maoni ya Kathpalia (1997) na Bhatia (2004) yalisaidia utafiti huu katika kueleza hatua mbalimbali katika ujenzi wa blabu.

Valor (2005) amefanya tafiti mbalimbali kuhusu blabu kwa kuegemea blabu za kidigitali. Alihakiki zaidi ya blabu sitini za kimtandao za vitabu vilivyochapishwa kati ya Septemba 2002 na Juni 2003 za Kampuni maarufu Uingereza za Uchapishaji za Wakati huo *(Penguin, Balllantino, Routledge, Barnes na Noble)*. Katika kazi hizi alionyesha sehemu tatu zinazounda blabu yaani maelezo (*description*), utathmini (e*valuation*) na kuhusu mwandishi (*about the author*). Katika maelezo, Valor (2005) anasema kuwa sehemu hii huweza kujumuisha maelezo mafupi ya yaliyomo kitabuni pamoja na ploti na wahusika. Kusudi lake kuu huwa kufahamisha wasomaji yaliyomo kitabuni.

Katika hatua ya utathmini,vifungu fulani vya maoni ya wasomaji huweza kutolewa kwenye magazeti au majarida. Wanaotoa maoni haya huwa wasomaji au waandishi wengine ambao husifia kitabu kwa wasomaji wengine. Katika hatua ya kuhusu mwandishi, kiwango cha masomo,maisha, kazi za awali, uraibu, familia na tuzo alizoshinda mwandishi hujumuishwa. Hatau hii hukusudia kuonyesha tajriba na weledi wa mwandishi. Aidha Valor aliibuka na modeli nyingine aliyoiita msogeo hatua ambapo alionyesha hatua sita za uandishi wa blabu ambazo ni utangulizi au maelezo, kuhusu mwandishi, utathmini, kuhusu kampuni ya uchapishaji, ujumbe au maudhui kutoka kitabuni na matarajio ya wasomaji. Modeli hii ya misogeo-hatua ndio msingi wa uchambuzi wa blabu katika utafiti huu.

Cacchiani (2007) alishughulikia lugha tathmini katika uandishi wa blabu. Alitaja hatua nne katika uandishi wa blabu. Hatua ya kwanza ni utambuzi ambao unajumuisha anwani, jina la mwandishi, jina la mchapishaji,nembo, msururu wa vitabu na nambari ya kimataifa ya kitabu. Hatua ya pili ni tajriba ya mwandishi ambayo hujumuisha bayografia ya mwandishi na tuzo alizoshinda. Hatua ya tatu ni dondoo kutoka kitabuni. Hii hujumuisha matini, wahusika, maoni kuhusu kitabu, mtindo na hadhira lengwa. Hatua ya nne ni kuthamini kitabu, ambayo hujumuisha mtindo na wakati mwingine hadhira lengwa.

Marčiulionienė (2006) anasema ingawaje blabu zinapaswa kuwa katika jalada la nyuma la kitabu, imetambuliwa kuwa blabu za vitabu vya kiingereza huwekwa kwenye sehemu mbalimbali za kitabu kama vile kwenye jalada la mbele, ndani mwa kitabu au kwenye kurasa tangulizi za kitabu husika. Alijitokeza na hatua tano katika uandishi wa blabu; Habari kuhusu kitabu, kuhusu mwandishi, kuhusu msururu wa vitabu vya mwandishi, kuhusu mchapishaji na maoni ya wataalamu.

Onderka (2013) alifanya utafiti wa blabu za kimtandao ambapo alichunguza blabu 95 za wauzaji wa vitabu za kidhana. Hii ilijumuisha blabu 40 za Kiingereza kutoka Amazon UK na 55 za Kituruki kutoka Okuoko TR. Aligundua kuwa blabu za Amazon zina Hatua 6 ambazo ni; kupongeza mwandishi, maelezo kuhusu kitabu, ithibati ya kitabu, kukuza kitabu, kuhusu mwandishi na tovuti ya mwandishi navyo vya Kituriki Okuok vilikuwa na hatua tano; kupongeza mwandishi, maelezo kuhusu kitabu,kumshirikisha mwandishi katika matini, matangazo kuhusu kitabu na mwandishi.

Japo tafiti nyingi huangazia vipengele vinavyojenga blabu kama vile habari kuhusu mwandishi, baadhi ya kazi za mwandishi na kadhalika, kuna pia vipengele vya kimshikamano vinavyopaswa kushughulikiwa na wataalamu. Valor (2005) aliwahi kudokeza maoni kuwa mbali na ujumbe kwenye blabu, vipashio vya kiisimu hufaa kuchambuliwa pia. Atai na Aghari (2017) wanasema kuwa kama muhtasari wa maneno yanayosifia kazi bunifu, blabu huwa na mtindo wa kipekee unaoweza kujumuisha matumizi ya msamiati uliyopigwa chuku, na sentensi mbalimbali ambazo lazima ziwe na athari fulani kwa msomaji. Aidha blabu huwa na mchango wa kisarufi ambao husaidia pakubwa katika uundaji wake.

Kulingana na Kirui (2021) mshikamano ni sifa ya kimatini kufasiriwa kama kitu kimoja bali sio kama sentensi zilizotengana. Sentensi huunganishwa katika matini na kufasiriwa kama kitu kimoja bali sio kama sentensi zilizotengana. Kwamba, uunganishaji huu hufanywa kupitia matumizi ya vipashio vya kiisimu ili kuonyesha uhusiano wa kimaana katika sentensi hizo. Aghalabu, mshikamano huchukuliwa kama umbo la nje ya matini na hujumuisha mshikamano wa kisarufi na

kileksika (Halliday & Hasan, 2014). Mshikamano kisarufi unajumuisha matumizi ya vipashio vya kisarufi kuunganisha sentensi katika matini ili kuonyesha uhusiano wa kimaana. Aina hii hutegemea ufasiri nje ya muktadha ambapo msomaji hajifungi katika matini ili kufasiri maana ya kitajwa kinachorejelewa (Kirui, 2021). Kwa mujibu wa Halliday na Hasan (2014), mshikamano wa kisarufi unahusu urejeshi (hasa wa kianafora), ubadilishaji, udondoshaji, na uunganishaji nao mshikamano kileksia hujumuisha sinonimu, antonimu, hiponimu na urudiaji.

## Nadharia ya Utafiti

### Nadharia ya Muundo Kipera

Nadharia ya Muundo Kipera (*Generic Structure Theory*) kwa mujibu wa Swales (1990) ilizingatiwa katika utafiti huu katika kuchambua blabu. Nadharia hii huonyesha uhusiano baina ya muundo wa matini na vipashio vyake faafu vinavyotumiwa kimuktadha katika kufaulisha madhumuni ya matini husika. Kimsingi, nadharia hii huwasilisha jumla ya vipengele vilivyo vya lazima na vile vya hiari, pamoja na mfuatano wake katika uundaji wa mwili wa matini ili matini yenyewe idhukuriwe kuwa faafu na kamilifu (Halliday, 1989). Nadharia hii ilishughulikia uchanganuzi wa vipashio faafu vinavyopatikana katika uandishi wa blabu za riwaya teule za *Utengano* (Mohammed, 2009) na *Chozi la Heri(* Matei, 2014*)*.

Muundo wa matini unaozingatiwa katika uundaji wa kipera maalum aghalabu huzingatia vipashio mbalimbali kama vile vipengele vya lazima (ambavyo lazima viwepo); vipengele hiari (ambavyo vinaweza kuwepo); mifuatano ya vipengele (mifuatano ipi ni lazima na ipi si lazima?); na mara ngapi vipengele hivi husika hutokea katika matini (Halliday & Hasan, 1989) Kutokana na nadharia hii, inabainika kuwa kila matini ina kipera chake maalum na kila kipera kina uwezo wake au uzuri wake. Hivyo basi, nadharia hii husaidia katika kubainisha matini faafu na zisizo faafu, kuonyesha namna muundo wa kipera kimoja kinavyofanana na kutofautiana na kingine na kuakisi utamaduni na msomaji hakiki wa matini (Kyaw & Zhiying, 2019). Kipera mojawapo chenye muundo maalum wenye vipashio vya lazima na hiari ni blabu.

Kamusi ya *Oxford Advanced Learners'* (1990) inafafanua blabu kama maelezo mafupi kuhusu yaliyomo kitabuni ambayo hupatikana katika jalada la nyuma la kitabu. Hata hivyo,Valor (2005) anaeleza zaidi kuwa blabu hazitoi tu maelezo kuhusu yaliyomo vitabuni bali pia hutathmini na kuonyesha vifungu mbalimbali kutoka kwa makala na magazeti ambayo husifia kitabu au mwandishi fulani. Hivyo basi, blabu huelezea habari kuhusu kitabu, hutumiwa kutathmini na kupendekeza kitabu kwa kukipongeza.

Blabu ndicho kipera ambacho kimechanganuliwa na wataalam kwa uzingativu wa nadharia ya Muundo Kipera. Kama anavyofafanua Al-Ali (2003) akimrejelea Labov (1972), nadharia ya Muundo Kipera husaidia hasa katika ufasiri wa misogeo katika miundo ya matini na pia vipashio vya kisarufi leksia vinavyotumiwa kubainisha msogeo huo husika. Japo Swales (1990) alizungumzia suala la msogeo katika uundaji wa blabu na kuhusisha vipashio kama vile maelezo ya kitabu,utathmini wa kitabu na kutoa habari kuhusu mwandishi, ufafanuzi wa nadharia hii aghalabu hufaulishwa kwa kutumia modeli iliyosahilishwa na Valor (2005) kama modeli ya msogeo-hatua (*Move-Step Model*).

Kulingana na modeli hii, kuna misogeo sita pamoja na hatua za kila msogeo zinazoweza kuzingatiwa katika uchanganuzi wa blabu kama vile: ufafanuzi/maelezo kuhusu kitabu, habari kuhusu mwandishi, utathmini, habari kuhusu mchapishaji, ujumbe/habari katika matini, na matarajio ya msomaji. Kila msogeo huwa na hatua zake. Misogeo hatua huchukuliwa kama mihimili ya nadharia ya Muundo Kipera. Msogeo wa kwanza ni Msogeo wa ufafanuzi au maelezo. Huu msogeo unahusisha hatua kama vile utangulizi wa kitabu, hadithi iliyoko na labda dondoo kutoka kitabuni. Ikumbukwe kwamba, msogeo wa maelezo ni lazima uwepo kwa blabu yoyote ile. Msogeo wa pili ni habari kuhusu mwandishi.

Katika sehemu hii, kuna hatua ya kutoa maelezo kuhusu familia, masomo/elimu , kazi zingine alizoandika , uraibu na tajriba yake. Pia mtindo wake wa uandishi huweza kurejelewa. Valor (2005) anasisitiza kuwa hatua ya maelezo kuhusu mwandishi ni lazima iwepo kwa blabu yoyote ile. Wakati mwingine hatua hii huweza kujumuisha kuongeza picha ya mwandishi kwenye blabu. Msogeo wa tatu unajumuisha utathmini ambao huhusisha hatua za utathmini wa kitabu, mtindo na pia mwandishi. Utathmini huweza kutokana pia na maoni ya wasomi wengine. Kimsingi, lengo kuu la sehemu hii ya utathmini ni kukisifia kitabu kwa hadhira ili iwe na motisha ya kutaka kukisoma. Sehemu ya utathmini inaweza kuwepo au isiwepo. Msogeo wa nne hujumuisha

habari kuhusu kampuni ya uchapishaji. Msogeo huu huwa na hatua ya kudhihirisha jina na nembo ya kampuni iliyochapisha kitabu.

Aidha, nambari ya kimataifa ya kitabu hujumuishwa. Hata hivyo, hatau hii si ya lazima (Valor, 2005). Msogeo wa ujumbe au maudhui kutoka kitabuni ndio msogeo wa tano. Hapa kuna mchakato wa kudokeza maudhui au ujumbe aliokusudia mwandishi kwa kifupi. Mafunzo kutoka kwenye kitabu hutolewa pia. Msogeo wa sita na wa mwisho huhusu matarajio ya wasomaji. Katika msogeo huu kuna hatua ya kutoa mapendekezo na maoni kuhusu kitabu ili msomaji aweze kushawishika. Aidha, maoni ya wasomaji au kampuni ya uchapishaji huweza kujumuishwa.

Mbali na masuala ya kimtindo katika blabu, masuala ya kimshikamano huweza kuangaziwa pia kwa mujibu wa Sari (2018) na Halliday na Hasan (2014) waliodokeza kuwa mshikamano unaweza kuwa wa kileksika (kuhusu urudiaji, sinonimu, hipanimu n.k) na pia kisarufi (kuhusu urejeshi, ubadilishaji, udondoshi na uunganishaji).


**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulikuwa wa kimaktaba ambapo kulikuwepo na usomaji wa kina wa riwaya ya *Utengano (*Mohammed, 2009*)* na *Chozi La Heri (*Matei, 2014*)*, tasnifu, makala, majarida na vitabu mbalimbali vinavyohusiana na mada na nadharia ya Semiotiki na Muundo Kipera.Usampulishaji wa makusudi ulitumika ambapo sampuli mbili ziliteuliwa; *Utengano(*Mohammed, 2009*)* na *Chozi La Heri (*Matei, 2014*)*. Data ilikusanywa maktabani kwa kutumia mbinu ya unukuzi ambapo orodha ya uchunzaji ilitumika kama kifaa katika kuelekeza unukuzi wa data faafu. Data iliyokusanywa ilithibitishwa kwa kurejelea riwaya teule ili kuhakikisha kuwa data hiyo ni sawa na yaliyomo katika riwaya teule na orodha ya uchunguzi.


Matokeo ya utafiti huu yaliwekwa wazi na mapendekezo kuhusu sehemu zinazoweza kufanyiwa utafiti baadaye zikapendekezwa. Data zilichanganuliwa kimaudhui kwa kurejelea madhumuni ya utafiti na nadharia ya Muundo Kipera na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo nathari. Maneno, maoni na kazi za waandishi mbalimbali zilizotumiwa katika utafiti zilitambuliwa. Aidha, utafiti haukupunguza wala kuongeza chochote kwenye kazi za vitabu vilivyotumiwa, kama njia ya kuzingatia hati miliki za watunzi.

**MATOKEO YA UTAFITI**

**Uchambuzi wa Vipashio vinavyojenga blabu**




**Kielelezo 1: Blabu ya riwaya ya *Utengano*(2009)**




**Kielelezo 2: Blabu ya riwaya ya *Chozi La Heri* (2014)**

**Misogeo Hatua**

Kulingana na Valor (2005) Hatua ya kwanza ya uandishi wa blabu huwa maelezo. Hatua hii hujumuisha utangulizi wa kitabu au hadithi iliyoko au dondoo kitabuni. Hatua hii imezingatiwa katika blabu za riwaya zetu teule. Mathalan, kuna dondoo katika blabu la riwaya ya *Utengano*:

> '*Mimi, mimi mwanao? Wewe nani?...Sogea hatua moja tu kama huitaki roho yako.Utanijua sasa hivi kuwa mimi siye tena Maimuna boza. Nyinyi ndio mlionibadilisha hivi. Nyinyi na dunia."* (Mohammed, 2009).

Aidha sehemu hii imezingatiwa katika blabu ya riwaya ya *Chozi La Heri:*

> "*Mungu Wangu! Huyu si ndugu yangu Mwaliko? Umu alisema kimyakimya. Dick naye alikuwa kaghumiwa hajui la kusema.Anamtazama mnuna wake kana kwamba ni Mr. Super Man katika sinema pendwa za kijasiri. Wote wawili walitazamana, kila mmoja akiapa moyoni kuwa amewahi kumwona kiumbe huyu mahali, lakini hakuna aliyethubutu kunena…"* (Matei, 2014).

Valor (2005) anasema kuwa sehemu hii ya utangulizi au maelezo ni lazima iwepo kwa blabu yoyote ile. Riwaya zote mbili zimezingatia hatua hii. Hatua ya pili hujumuisha habari kuhusu mwandishi ikiwemo familia, masomo, tajriba au kazi zingine za mwandishi. Cacchiani *(2007)* anaongezea kwamba tajriba ya mwandishi ambayo hujumuisha bayografia ya mwandishi na tuzo alizoshinda huweza kujumuishwa. Katika riwaya ya *Utengano*, tajriba ya mwandishi imetajwa:

> *Said Ahmed Mohamed ni mwandishi mashuhuri aliyebarikiwa na ukwasi wa lugha ya Kiswahili* (Mohammed, 2009).

Tajriba ya mwandishi wa *Chozi La Heri* pia imetajwa:

> *Asumpta K. Matei ni mtafiti na mwalimu mwenye tajriba pana katika ufundishaji wa lugha na fasihi ya Kiswahili katika Shule za Upili na Vyuo vikuu. Kati ya Taasisi alizowahi kufundisha ni Kenya High School na Catholic University of Eastern Africa. Ameshiriki katika majopo mbalimbali ya ukuzaji na utekelezaji wa mitaala* (Matei, 2014).

Kuhusu kazi zingine za mwandishi.

> '*Baadhi ya vitabu vyake vingine vilivyochapishwa na Longhorn ni Misemo, Milio na Tashbihi, Vito Vya Hekima, Dunia Mti Mkavu, Arusi ya Buldoza, Sikate Tamaa na Jicho La Ndani.'* (Mohammed, 2009).

Hatua ya nne ya uandishi wa blabu ni kuhusu kampuni ya uchapishaji. Hapa jina la kampuni hutajwa. Katika riwaya ya *Utengano*, kampuni ya uchapishaji imetajwa; *Longhorn Publishers*. Aidha nambari ya kimataifa ya uchapishaji imejumuishwa katika riwaya hii:

> *ISBN 9966497031* (Tazama Kielelezo 1).

Katika riwaya ya *Chozi La Heri* pia kampuni ya uchapishaji imetajwa; *One Planet*. Aidha nambari ya kimataifa imejumulishwa katika hatua hii:

> *ISBN 9789966068439* (Tazama Kielelezo 2).

Valor (2005) anasema kuwa hatua hii sio lazima. Hatua ya tano hujumuisha ujumbe au maudhui kutoka kitabuni.Ujumbe huu hudokezwa kwa kifupi. Mathalan katika riwaya ya *Utengano:*

> *Maimuna-Mwari Mwarika, mwana wa nyumba kubwa-kabadilika kiasi hicho? Ni nini hasa kilicholeta Utengano nyumbani mwa Bw. Maksuudi?* (Mohammed, 2009).

Katika blabu ya riwaya ya *Chozi La Heri* , ujumbe uliomo kitabuni umeelezwa kwa kifupi:

> *Tamaa ya kumiliki nyenzo za kujiinua kiuchumi na kisiasa kama inavyodhihirika katika riwaya hii inasambaratisha asasi za kijamii, pamoja na miundomsingi asasi za mshikamano wa kijamii. Maazimio yasiyofikiwa yanazua hali ya kuvunjikiwa kihoro hasa. Lakini baada ya kiza kizito huja mawio ya usawa wa jamii mpya yenye matumaini* (Matei, 2014).

Riwaya teule zimezingatia hatua ya kwanza ya ufafanuzi au maelezo, hatua ya pili kuhusu mwandishi, hatua ya nne kuhusu kampuni ya uchapishaji na hatua ya tano kuhusu ujumbe au maudhui kutoka kitabuni.

**Mshikamano**

Kulingana na Kirui (2021) mshikamano ni sifa ya kimatini kufasiriwa kama kitu kimoja bali sio kama sentensi zilizotengana. Mshikamano unadhukuriwa kama umbo la nje ya matini na hujumuisha mshikamano wa kisarufi na kileksika (Halliday & Hasan, 2014). Mshikamano kisarufi unajumuisha matumizi ya vipashio vya kisarufi kuunganisha sentensi katika matini ili kuonyesha uhusiano wa kimaana. Mshikamano wa kisarufi unahusu urejeshi (hasa wa kianafora), ubadilishaji, udondoshaji, na viunganishi vinavyotumiwa katika matini.

**Urejeshi**

Kirui (2021) anasema urejeshi ni uhusiano baina ya ishara za kiisimu na kile kinachowakilishwa katika ulimwengu au ulimwengu wa diskosi au katika matukio fulani ya tamko. Ili kuelewa maana katika sentensi au aya moja ni lazima kwa msomaji kurejelea sentensi iliyotangulia katika matini. Kunao urejeshi endofora ambao huonyesha ufasiri wa maana ya kipashio umo katika matini, ambapo kitu kinachorejelewa kinaweza kutambulika katika matini.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (*Matei, 2014*)* kunao urejeshi katika dondoo kwenye blabu.

> '…*Wote wawili walitazamana*…'

neno '*wote*'katika muktadha huu linarejelea Dick na Umu ambao tayari walikuwa washatajwa. Ili kuelewa maana ya 'wote'', msomaji anafaa kurejelea ujumbe wa awali. Pia katika riwaya ya *Utengano (*Mohammed, 2009*)*, kuna urejeshi endofora katika dondoo kwenye blabu:

> *…'Nyinyi ndio mlionibadilsiha hivi. Nyinyi na dunia…'*

Neno '*nyinyi*' linarejelea Mussa na Maksudi. Ili kuelewa kile ambacho neno '*nyinyi*'linarejelea msomaji anafaa kusoma habari zilizotangulia sentensi hii.

**Uunganishaji**

Matei (2008) anaeleza uunganishaji kama matumizi ya neno, fungu la maneno au viambishi kuunganisha na kuonyesha uhusiano baina ya sentensi mbili au zaidi. Wesana-Chomi (2017) wanashikilia kuwa viunganishi ni vipashio ambavyo huweka pamoja sehemu mbalimbali za sentensi ili kuzifanya ziwe kipashio kimoja kikuu. Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa viunganishi hutumika kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini. Kulinganan nao, kuna viunganishi kama vile viongezi, vya kuonyesha sababu, kinyume, chaguo, masharti na vitegemezi.

Katika blabu ya riwaya ya *Chozi la heri* (Matei, 2014), kuna viunganishi ambavyo vimetumiwa kuunganisha sentensi kuonyesha uhusiano kimaana

> '*Wote wawili walitazamana, kila mmoja akiapa moyoni kuwa amewahi kumwona kiumbe huyu mahali, lakini hakuna aliyethubutu kunena…'* (Matei, 2014).

Kiunganishi kilichotumika ni '*lakini'* ambapo kinaonyesha mpishano wa kinyume wa hali mbili; wahusika wanatazamana.Hakuna anayechukua hatua ya kumzungumzia mwingine. Kiunganishi kimetumiwa kuonyesha ukinzano katika matini.

**Udondoshaji**

Huhusisha kuacha baadhi ya maneno ili kuepuka urudiaji. Nafasi huweza kujazwa kwa kurejelea vipashio katika sentensi iliyotangulia ili kupata neno lililofaa kuchukua nafasi hiyo.

Katika blabu ya riwaya ya *Chozi la heri (*Matei, 2014*)* kuna udondoshaji katika dondoo;

> '*Dick naye alikuwa kaghumiwa, hajui la kusema. Anamtazama mnuna wake kana kwamba ni…'*

Sentensi hii ingalikuwa*, 'Dick naye alikuwa kaghumiwa, Dick hajui la kusema. Dick anamtazama mnuna wake kana kwamba…*'Ili kuelewa kitendo '*hajui la kusema'*, na '*anamtazama mnuna wake…*' msomaji lazima arejelee '*kitendo kaghumiwa'* (ambaye ni Dick). Udondoshaji huonyesha uhusiano wa kisarufi kati ya maneno ambapo jambo ambalo limeeleweka linatumika kwa njia fulani bila kutamka au kusema (Halliday & Hasan, 1978).

**Ubadilishaji**

Neno au kirai kuchukua nafasi ya neno au kirai kingine katika sentensi. Kirui (2021) anasema kuwa ubadilishaji huchunguzwa kwa sababu ufasiri wa maana ya maneno ambayo nafasi yao imechukuliwa na maneno mengi katika matini humhitaji msomaji kurejelea maneno yaliyotajwa katika sentensi zilizotangulia.

> '*Ilikuwaje hata Maimuna-mwari mwarika, mwana wa nyumba kubwa-kabadilika kiasi hicho?*(Mohammed, 2009).

Kifungu '*mwana wa nyumba kubwa'* kinamrejelea Maimuna na ili msomaji kuelewa kifungu hiki anafaa kurejelea jina *Maimuna.*

**Hiponimu**

Ni matumizi ya maneno ambayo maana ya neno moja huwa sehemu ya maana ya neno lingine.

Katika blabu ya riwaya ya *Chozi la Heri (*Matei, 2014*)*, kuna matumizi ya haiponimu katika dondoo kutoka riwayani;

> *'Mungu wangu! Huyu si ndugu yangu Mwaliko?' Umu alisema kimya kimya. Dick naye alikuwa kaghumiwa, hajui la kusema. Anamtazama mnuna wake kana kwamba…'*

Neno *mnuna* lina maana ya ndugu mdogo wa kiume au kike. Neno *mnuna* lina maana ndogo na hupatikana chini ya mwavuli wa neno *ndugu*. . Hivyo neno ndugu lina uhusiano wa kihaiponimu na neno *mnuna.*

**Maudhui kutokana na Misogeo-Hatua Mabadiliko**

Katika blabu ya riwaya ya *Utengano (Mohammed, 2009)*, dondoo kutoka kitabuni linaafiki maudhui ya mabadiliko;

> '*Mimi, mimi mwanao? Wewe nani?... Sogea hatua moja tu kama huitaki roho yako.Utanijua sasa hivi kuwa mimi siye tena Maimuna boza. Nyinyi ndio mlionibadilisha hivi. Nyinyi na dunia."* (Mohammed, 2009*)*.

Maimuna anawarejelea kakake Mussa na babake Maksuudi ambao anadai wao na dunia ndio waliombadilisha. Kuna matukio kadhaa katika riwaya hii yanayoashiria mabadiliko. Mhusika Mussa alikuwa kijana aliyependa anasa lakini baadaye anabadilika na kuacha anasa .Anajitahidi masomoni hadi kuhitimu chuo kikuu na hata kupata mke, Sihaba.

Maimuna pia alikuwa msichana mtiifu chini ya utawa wa babake lakini mwishowe anatoroka kwao na kubadilika hadi kuwa kahaba na mlevi kule Bobea na Pumziko. Hata hivyo, anapokutana na Kabi wanapendana na kuoana. Maimuna anayaasi maisha ya anasa na kumpenda mumewe na kuwa mke mchapa kazi.

Bwana Maksuudi pia anapitia mabadiliko katika maisha. Kwanza, hapo mwanzo alikuwa fukara. Alijiunga na wapiganaji uhuru wenzake kupigania uhuru wa nchi yao lakini alipopata mali babada ya uhuru alianza kuwatesa na kuwadharau maskini. Pia aliwanyang'anya mali zao na kufanya biashara za magendo na wageni. Aidha anawanyayasa wanafamilia yake kwa kuwapiga na kuwatawisha. Baada ya kutoka jela alikokuwa amefungwa kwa miaka miwili, Maksuudi anarudi kuwa maskini na bila familia. Hali hii inamfanya kumtafuta mkewe aliyemtaliki kumuomba msamaha na kuwatafuta wanawe.

Bi Farashuu pia anaonyesha mabadiliko. Mwanzoni alikuwa amejawa na kisasai dhidi ya familia ya Bwana Maksuudi kwa kuteswa kwa mwanawe Biti Sururu. Baadaye anabadilika na kuibariki ndoa ya Maimuna na mjukuu wake Kabi. Aidha anasikitishwa na kifo cha Maksuudi. Hatua ya nne kuhusu ujumbe uliomo kitabuni inadhihirisha ujumbe mkuu aliotaka kuwasilisha mwandishi; Utengano

> *Maimuna-Mwari Mwarika, mwana wa nyumba kubwa-kabadilika kiasi hicho? Ni nini hasa kilicholeta Utengano nyumbani mwa Bw. Maksuudi?*( Mohammed, 2009*).*

Kulingana na kamusi ya Kiswahili Sanifu ya karne ya 21, utengano ni  hali ya kuondoka au kujitenga kutoka kwa kikundi, mtu au hali yao ambayo mbeleni mtu alikuwa amehusika nayo. Pia ni hali ya kutokuwa pamoja au kuelewana. Utengano mbalimbali unadhihirika katika riwaya hii.

**Utengano kifamilia**

Utengano wa kwanza ni talaka kati ya Bw. Maksuudi na mkewe wa kwanza Mwanasururu, bintiye Farashuu. Tunaelezwa msingi wa utengano huu ni tamaa na ubinafsi wa Bw. Maksuudi, mambo yaliyompelekea kufisidi mali aliyorithi bibi huyo kutoka kwa babake. Mathalan, Kabi akimweleza Maimuna yalimsibu amamke, Mwanasuru anasema:

> *Basi bwana huyo aliviwania kwa hadaa na hadaa iliposhindwa alitumia mabavu. Alipokwisha vipata tu, alimwacha mama* (*Mohammed, 200, p. 164*).

Alimtesa kisha akaachana naye na akafa kwa mateso alikoenda. Hii ndio sababau iliyomfanya Farashuu kuwa na machungu na Maksuudi na kuapa kulipiza kisasi. Kwa kutumia Kazija, Farashuu alimfumanisha Maksuudi na Mussa, mtu na mwanawe, nyumbani kwa Kazija, wakisaka mapenzi na kusababisha mwana na baba kutengana. Kwa kutumia Biti Kocho, Farashuu alisambaratisha familia ya Maksuudi hadi wakatalikiana na mkewe, na kitoto kichanga kikafa baadaye. Aidha alisababisha kutoroka kwa Maimuna kutoka kwao. Hivyo, wanafamilia ya Maksuudi wakatengana wote wasionane na kushirikiana kwa muda mrefu.

Kunao utenganao baina ya ndugu wa toka nitoke, Maksuudi na Inspekta Fadhili. Hii inasababishwa na misimamo yao kinzani kuhusu sera za maisha. Maksuudi ni fisadi na mpotovu wakati Fadhili ni mwadilifu na mwongofu katika utendakazi wake. Wanapokutana hawaelewani bali wanakosana. Utengano huu unapelekea Fadhili kumnasa Maksuudi kwa kosa la jinai na kumtumbukiza gerezani kwa miaka mawili. Undugu unaisha na kubakia uhasama. Utengano wa kifamilia unasababishwa na tabia mbaya ya Maksuudi ya kuwatenda waja vibaya na kuwanyanyasa.

Katika *Chozi la Heri* (Matei, 2014 ) familia ya Kaizari na Subira inasambaratika wanapoachana kutokana na mama mkwe kumkataa Subira kwa sababu za kikabila.

**Utengano na utu**

Utengano huu unabainika katika vitendo vilivyo kinyume na utu na ubinadamu. Maksuudi alithamini sana mali na kuwadharau waliomuinua. Aliwatesa wanawake na kuwanyima uhuru wao. Kwa mfano;

> *Maksuudi aliwaza aliowatendea vibaya. Aliwavuta akilini wote alioweza kuwakumbuka lakini alipofika kwa Mwanasururu, aliyekuwa mkewe, alikataa kuwaza zaidi. Aliyomtendea Mwanasururu ulikuwa unyama (Mohammed, 2009, p. 4).*

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (*Matei, 2014)  kunavyo vitendo vya wahusika ambavyo vinakiuka ubinadamu. Kwa mfano, kuna wale wanaonyayanyaswa kimapenzi. Mwanaharakati analalamikia kulawitiwa kwa wavulana.Mwanaheri na Lime wanabakwa  na vijana wenzao naye Sauna anabakwa na baba yake wa kambo.

**Utengano kijinsia**

Jamii hii inaonekana kujengeka katika mfumo wa kuumeni. Huu ni mfumo unaompendelea mwanamume na kumdunisha mwanamke. Katika riwaya hii wanawake wamenyimwa uhuru na wanaume. Wengi wanaonekana wakitawishwa huku wanaume wakimiliki nafasi bora katika jamii, amabapo wana uhuru wa kufanya lolote wapendalo. Maksuudi anawatawisha mkewe Tamima na bintiye Maiumuna. Hawaruhusiwi kutoka nje wlaa kumkaribisha mtu yeyote pasi idhini ya Maksuudi. Tamima ananyimwa uhuru wa kujichagulia mkunga wala kwenda hospitalini kujifungua. Pia hana haki ya kukataa talaka kisheria au kiukoo. Selume ananyanyaswa na mumewe Shoka lakini hawezi kuacha ndoa kwa sababu mumewe hayupo tayari kumpa talaka. Shoka anamwambia;

*'Mimi sikwachi talaka, nitakwacha utimbwe na ulimwengu wako* (Mohammed, 2009, p. 122*)*.

Wanaume wana elimu bora, kazi bora na uongozi hasa wa kisiasa. Kwa mfano, Mussa anasoma hadi chuo kikuu na kuhitimu kuwa daktari. Maksuudi na Zanga ni viongozi wakubwa naye Fadhili ni Inspekta wa polisi. Kwa upande mwingine, wanawake wanaendesha shughuli ndogo ndogo za kuchumia riziki kama vile kuoka mandazi, kuendesha madanguro na kupika pombe ya kienyeji. Mathalan, Mama Jeni na Biti Sururu wanaendesha biashara ya madanguro kujipatia riziki. Maimuna na Kazija wanashiriki ukahaba kama njia ya kujikwamua kiuchumi.

**Utengano kitabaka**

Maksuudi anawakilisha tabaka la matajiri na wanawake wote wanawakilisha tabaka la maskini. Matajiri kama vile Maksuudi wanaishi katika majumba makubwa makubwa huku maskini wakiishi katika maeneo duni ya vichochoroni. Maksuudi anaishi Liwazoni ambapo kuna Kasri nzuri.

Katika riwaya ya *Chozi La Heri* (Matei, 2014) hatua ya nne inadhihirisha mambo kadhaa ambayo mwandishi alikusudia kuwasilisha; tamaa na ukabila.

> *Tamaa ya kumiliki nyenzo za kujiinua kiuchumi na kisiasa kama inavyodhihirika katika riwaya hii inasambaratisha asasi za kijamii, pamoja na miundomsingi asasi za mshikamano wa kijamii. Maazimio yasiyofikiwa yanazua hali ya kuvunjikiwa kihoro hasa. Lakini baada ya kiza kizito huja mawio ya usawa wa jamii mpya yenye matumaini* (Matei, 2014).

**Tamaa**

Viongozi wa taasisi mbalimbali za umma wananyakua ardhi ya msitu hadi kuwaacha wanyama bila makao. Aidha viongozi wa shirika la maghala ya nafaka wanawauzia wananchi mahindi yaliyoharibika kwa sababu ya tamaa. Tamaa ya pesa inamfanya Buda kumwingiza Dick katika biashara ya ulanguzi wa dawa za kulevya akiwa na umri mdogo. Walinda usalama nao wana tamaa ya pesa ambapo wanachukua hongo na kumruhusu Buda kuendeleza biashara yake haramu ya uuzaji wa dawa za kulevya.

**Ukabila**

Hii ni hali au tendo la mtu kuthamini kabila lake na kuliona la mwingine likiwa duni na hivyo kulidhalilisha. Mwandishi wa riwaya hii ameonyesha namna ukabila unavyoharibu amani na ukuaji katika jamii. Ukabila unaleta utenganao. Mathalan, Ridhaa anatengwa na wenzake shuleni, hadi kukataa kucheza naye kwa kisingizio kuwa yeye sio mzaliwa wa Msitu wa Heri. Jambo hili linampa matatizo ya kisaikolojia.

Wakati wa vurugu ya vita baada ya uchaguzi, Selume anatoroka kwake kwa kuwa yeye ni wa kabila tofauti na mumewe. Mume wake baadaye anaoa msichana wa kabila lake. Mwandishi pia ameonyesha kuwa ukabila huleta uharibifu wa mali. Mathalan, majirani wa Ridhaa wanateketeza nyumba na familia yake licha ya kuwa ni watu ambao amekuwa akiwafadhili.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho**: Makala hii imeonyesha kuwa blabu kama mtindo hujumuisha hatua za kimtindo na kiisimu katika ujengwaji wake. Hatua zilizobainishwa katika blabu za riwaya teule ni hatua ya kwanza ya ufafanuzi/maelezo, hatua ya pili kuhusu mwandishi, hatua ya nne kuhusu kampuni ya uchapishaji na hatua ya tano kuhusu ujumbe kutoka kitabuni. Maudhui yaliyobainishwa kutokana na hatua hizi ni pamoja na mabadiliko, utengano, tamaa na ukabila. Aidha kipengele cha kiisimu cha mshikamano katika kujenga blabu kilibainisha elementi za urejeshi, uunganishaji, ubadilishaji, udondoshaji na haiponimu. Makala imethibitisha kuwa msanii anaweza kutumia blabu kama mtindo katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake.

**Mapendekezo:** Mtafiti anapendekeza kuwa watafiti wa baadaye watafiti mitindo katika blabu za tamthilia.

**REFERENCES**


Adhikary, B. (2012). A study on book blurbs: Quest for a new tool as well as a new record for the library.

Al-Ali, M. N. (2003). Analyzing the generic structures and the rhetorical patterns of the Quranic narrative parables. *Al-'Arabiyya, 36,* 81–106.

Assumpta, K. M. (2014). *Chozi la heri*. One Planet Publishing and Media Services Limited.

Atai, M., & Aghari, M. (2017). Exploring disciplinary variation in the generic structure and metadiscourse features of online academic book blurbs. *Ampersand.*

Banari, R., Jalilifar, A., & Shooshtari, Z. G. (2019). Exploring the patterns of evaluative language in applied linguistics blurbs: A rhetorical structure analysis. *Teaching English Language, 13*(1), 205–233.

Bhatia, V. K. (2014). *Analysing genre: Language use in professional settings.* Routledge.

Burghes, G. (1906). *Are you a bromide?* Huesbsch.

Cacchiani, S. (2007, July). From narratives to intensification and hyperbole: Promotional uses of book blurbs. In *Proceedings of the Corpus Linguistics Conference,* University of Birmingham (Vol. 27, p. 30).

Habwe, J. H., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili.* Phoenix.

Halliday, M. A. K. (1978). *Language as social semiotic.* Arnold.

Halliday, M. A. K., & Hasan, R. (1989). *Language, context, and text.* Oxford University Press.

Halliday, M. A. K., & Hasan, R. (2014). *Cohesion in English.* Routledge.

Kathpalia, S. S. (1997). Cross-cultural variation in professional genres: A comparative study of book blurbs. *World Englishes, 16*(3), 417–426.

Kirui, S. K. (2021). *Urejelezi katika gazeti la Taifa Leo: Mtazamo wa kipragmatiki* [Doctoral dissertation]. University of Nairobi.

Kitula, K. (2001). *Mwongozo wa Kiu.* Sasa Sema Publishers.

Kitula, K. (2008). *Mwongozo wa Utengano.* Sasa Sema/Longhorn.

Kyaw, A. M., & Zhiying, X. (2019). Exploring generic structure potential of selected editorials in the Myanmar Times newspaper. *Language Literacy: Journal of Linguistics, Literature and Language Teaching, 3*(2), 139–149.

Labov, W. (1972). Some principles of linguistic methodology. *Language in Society, 1*(1), 97–120.

Marčiulionienė, V. (2006). Publisher's blurb on English books of fiction: A diachronic genre analysis. *Filologija, 11,* 61–71.

Matei, A. K. (2008). *Darubini ya sarufi: Ufafanuzi kamili wa sarufi ya Kiswahili: Maswali na mazoezi.* Phoenix Publishers.

Mathenge, J. (2006). *Mwongozo wa Kifo Kisimani.* Top Achievers.

Matthews, B. (1922, September 24). A round-up of blurbs. *The New York Times.*

Mohammed, S. A. (2009). *Utengano.* Longhorn Publishers.

Ogato, M. (2018). *Nafasi ya mshikamano katika kukuza maudhui katika insha za wanafunzi wa kidato cha nne katika Kaunti ya Murang'a* [Doctoral dissertation]. Kenyatta University.

Ogunsiji, A. (2007). Aspects of the phono-graphological design in Soyinka's "Faction." *Nebula, 4*(3).

Önder, N. (2013). Generic structure and promotional elements in best-selling online book blurbs: A cross-cultural study. *Ibérica: Revista de la Asociación Europea de Lenguas para Fines Específicos (AELFE), 25,* 171–194.

OALD. (1990). *The Oxford Advanced Learner's Dictionary.* Oxford University Press.

Sari, M. K. (2018). The distinctive linguistic features in blurbs as found in non-fictions: A stylistic analysis. *Jurnal KATA, 2*(1), 150–158.

Saunders, M., Lewis, P., & Thornhill, A. (2009). *Research methods for business students* (5th ed.). Prentice Hall.

Swales, J. M. (1990). *Genre analysis: English in academic and research settings.* Cambridge University Press.

Swick, C. L. (1939). The book blurb. *The English Journal, 28*(2), 140–142.

Tanaka, K. (2005). *Advertising language: A pragmatic approach to advertisements in Britain and Japan.* Routledge.

Thompson, H. (2017). The French metanarrative of blindness. In *Reviewing blindness in French fiction, 1789–2013* (pp. 17–39). Palgrave Macmillan.

Valor, M. L. G. (2005). Advertising books: A linguistic analysis of blurbs. *Ibérica: Revista de la Asociación Europea de Lenguas para Fines Específicos (AELFE), 10,* 41–62.

Valor, M. L. G., & Ros, M. I. (2009). On the dynamic nature of genre: A diachronic study of blurbs. In *Academic evaluation: Review genres in university settings* (pp. 199–216). Palgrave Macmillan.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia.* Focus Publishers.

Wesana-Chomi, E. (2017). *Kitangulizi cha muundo viambajengo wa sentensi za Kiswahili* [Doctoral dissertation]. University of Dar es Salaam.